**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**

**SIMU**
H/M: **0784784518**
S/M **0785803250**
A/M: **0786180854**

SHULE YA SEKONDARI BUKAMA,
S. L. P 01,
**SHIRATI-RORYA.**
TAREHE: 19/05/2022

KUMB. NA. BSS/JOI/F. V/2022

NDUGU: Mzazi/Mlezi wa ……………………………………
…………………………………………………………………
S. L. P ………………………………………………………..

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUKAMA MWAKA 2022**

1. **UTANGULIZI**

Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu.
Ni matumaini yetu kuwa utatumia vizuri nafasi hii kwa kusoma kwa bidii, kuwa na nidhamu na kutumia maarifa yako yote ili kufikia malengo yako kielimu na hatimaye kuwa raia mwema anayetegemewa na jamii, taifa, na ulimwengu kwa ujumla.

2. **MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Bukama ipo Wilaya ya Rorya Mkoa wa Mara. Kwa watakaotoka Mwanza au Musoma wapande mabasi yanayoenda **Tarime,** kwa Mwanza mabasi hayo yanapatikana katika stendi ya **Buzuruga Mwanza** na kwa Musoma mabasi hayo yanapatikana stendi ya Bweri washuke **Tarime stendi** Kisha wapande magari yanayoelekea Shirati kupitia **Bukama** Gharama ya kutoka Tarime hadi Bukama centre au kibao cha shule ya sekondari Bukama ni Tsh.5,000/=tu.
Kwa wanaotokea Tarime wapande magari yanayoelekea Shirati kupitia Bukama na washuke Bukama centre au kibao cha shule ya sekondari Bukama**,**
Kutoka kibao cha sekondari ya Bukama ni umbali wa mita 200 hadi kufika shuleni ambapo watatembea kwa miguu.

3. **KUFUNGUA SHULE**

Shule itafunguliwa siku ya ………………………… kuanzia saa 1:00 asubuhi. Siku hiyo ufike shuleni ukiwa na mahitaji yako yote muhimu ya shule. Tambua kuwa kama utashindwa kuripoti shuleni ndani ya wiki mbili tangu shule ifunguliwe nafasi yako atapewa mwanafunzi mwingine. Mara mwanafunzi afikapo shuleni aripoti katika ofisi ya **Makamu** Mkuu wa shule kwa mapokezi na usajili, afike na nakala ya **hati ya kuzaliwa ya serikali** (Birth Certificate) pamoja na **Result Slip** ya kidato cha nne pamoja na **stakabadhi halisi** ya Michango aliyolipia benki.

4. **KARO NA MICHANGO MINGINE YA SHULE**

Mwanao anatakiwa kulipia ada na michango mingine ya shule kama ilivyoainishwa hapa chini kwenye orodha ya mahitaji **na 5A** na sio vinginevyo. (Hatutapokea fedha ambazo zinatakiwa zilipwe benki). Malipo yote yalipwe benki na yafanyike kwa kutumia jina la mwanafunzi tu. Karo na michango yote ilipwe kwenye Akaunti **Na. 30 40 1 00 0024 NMB.** Jina la Akaunti ni**Bukama Secondary School.** Fedha zinazotakiwa kuwekwa akaunti hii ni Karo, Mchango wa taaluma, Miundo Mbinu, Walinzi na Wapishi. Fedha ya bima na huduma ya kwanza aje nayo mwanafunzi.

Ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza kwa kutokamilisha michango yote ya shule, hakikisha kwamba unakamilisha michango na mahitaji yote ya shule. Baada ya malipo wasilisha risiti halisi ya malipo shuleni kwa Mhasibu wa shule.

Ndugu Mzazi/Mlezi, shule hii haitoi kabisa chakula tofauti na kile kinachotumiwa na wanafunzi wote kwa mwanafunzi mmoja mmoja **(Special Diet).** Vyakula vinavyotumika hapa shuleni ni Ugali Maharage, Wali Maharage, pia nyama kwa kadri ya ratiba yao atakavyoikuta hapa shuleni.

Pamoja na barua hii naambatanisha orodha kamili ya Nyaraka muhimu ambazo anatakiwa kuja nazo zikiwa zimefanyiwa kazi kwa umakini zaidi.

A. Fomu ya sheria na taratibu za shule. Mwanafunzi azisome na kuzielewa kabla hajajiunga na shule yetu.
B. Fomu ya Historia ya mwanafunzi – ijazwe na iwasilishwe shuleni.
C. Hati ya kiapo cha kukubali kujiunga na shule na kiapo cha mzazi –ijazwe na iwasilishwe shuleni.
D. Fomu ya vipimo vya Afya ya mwanafunzi - Apimwe na majibu yawasilishwe shuleni.

5. **ORODHA KAMILI YA MAHITAJI YA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI:**

**A.**Fedha taslimu ambayo inatakiwa iwekwe benki halafu awasilishe Stakabadhi ya Malipo (Pay in Slip) katika Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule.

1. Karo ya shule **Tsh. 35,000/=**kwa muhula mmoja au **Tsh. 70,000/=** kwa mwaka.
2. Michango kwa malipo ya walinzi na wapishi **Tsh. 60,000/=** kwa mwaka.
3. Fedha za Matibabu **Tsh. 10,000/=**kwa mchanganuo kwamba ni mchango wa huduma ya kwanza **Tsh. 5,000/=** na Bima ya afya **Tsh. 5,000/=** kama mwanafunzi ana bima atatoa **Tsh. 5,000/=** ya huduma ya kwanza peke yake, aje nayo mkononi.
4. Mchango wa tahadhari Tsh. **10,000/=** (Hairudishwi).
5. Taaluma Tsh. **10,000/=** kwa muhula.
6. Kitambulisho na Picha Tsh. **6,000/=** aje nayo mkononi
7. Ukarabati wa samani Tsh. **20,000/=** kwa mwaka aje nayo yote mkononi siku ya kuripoti
8. Nembo ya shule Tsh. **2000/=** aje nayo mkononi.

B. **SARE ZA SHULE:**

1. Suruali mbili (02) rangi ya khaki moja na ughoro moja zenye marinda mawili pande zote, mifuko mitatu (mmoja wa nyuma na miwili ya mbele). Ashone aje nazo
2. Shati mbili (02) au zaidi nyeupe za MIKONO MIREFU na zenye mfuko mmoja tu, aje nazo (Shati daima itachomekwa ndani ya suruali ivaliwapo kadhalika na T-shirt.
3. T-shirt mbili (02) za kushindia zenye kola zinapatikana shuleni kwa bei ya 15,000/=@
4. Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba jozi mbili (02) visiwe na visigino virefu na muundo wa 'boot', aje navyo.
5. Soksi nyeusi jozi nne (04) na zisiwe na mistari au madoadoa aje nazo.
6. Sweta mbili za kuvaa (Special) wakati wa baridi **rangi moja khaki na nyingine ughoro** aje nazo
7. Mkanda mweusi wa kiuno (Upana inchi 1.5) kufungia suruali.
8. Bukta na fulana ya bluu kwa ajili ya michezo.
9. Viatu vya raba vya michezo na shughuli za nje.
10. Track suit nyeusi /blue aje nayo.
11. Suruali ya kushindia ya rangi nyeusi iwe na marinda mawili pande zote mbili. Mguu inchi 16. (Ndio avae siku ya kuripoti asije kabisa na nguo ya nyumbani).
12. Viatu vya wazi (Open Shoes) vitavaliwa baada ya vipindi vya darasani.
13. Tai mbili (02) rangi moja yenye ughoro na nyingine yangi ya khaki.

NB; Mwanafunzi hatakiwi kuja na mavazi au vitu vingine ambavyo havijaelekezwa katika form hii.

C. **VIFAA VYAKE VYA KUTUMIA BWENINI:**

1. Godoro la 'Sponge' la upana wa futi 2.5 x 6 aje nayo.
2. Shuka mbili (02) rangi ya blue bahari (light blue) na pinki aje nazo.
3. Ndara/Kanda mbili aje nazo.
4. Sanduku la bati na kufuli kwa ajili ya kutunza vitu vyake (ni lazima) aje nayo.
5. Chandarua rangi ya bluu, aje nacho.
6. Ndoo ya kuchotea maji ya lita ishirini (20) aje nayo.
7. Ndoo ndogo ya kuogea ya lita kumi (10).
8. Taulo aje nayo.
9. Dumu la lita tano la kutunzia maji ya kunywa aje nayo.
10. Toilet paper tano kwa ajili ya matumizi yake aje nazo zitakaguliwa.
11. Sahani, bakuli, kijiko na kikombe cha nusu lita, aje navyo.
12. D-light ndogo ya **Solar** ya kutumia umeme ukikatika.
13. Pia usisahau kumpa mwanao fedha za kutoshakwa ajili ya matumizi yake binafsi.
14. Blanketi kwa ajili ya kujifunika wakati wa baridi.

Mzazi/Mlezi kumbuka kwamba, ili mwanafunzi aweze kufikia malengo yake ya kitaaluma, anapaswa pia awe anasoma vitabu. Shule haina vitabu vya kutosha. Hivyo basi, unaagizwa na BODI YA SHULE kumnunulia mwanao vitabu visivyopungua vitano vya masomo tofauti kati ya masomo hayo ni:- (i) Economics. (ii) Hesabu (BAM) (iii) pure mathematics (iv) History (v) Jiografia. (Geography) (vi)General Studies.

D.**<u>VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI:</u>**

1. Ream mbili (02) ya karatasi za photocopy (Double A) aje nayo. .
2. Madaftari makubwa CounterBooks Quire 3, au Quire 4 yasiyopungua saba (7) na pia daftari ndogo ya mazoezi yasiopungua (07) aje nayo.
3. Flat file moja.
4. Graph Pad 02.
5. Mathematical set.

E. **<u>VIFAA VYA KUFANYIA USAFI</u>:**

1. Reki yenye mpini moja aje nayo.
2. Jembe na mpini wake aje nalo.
3. Ufagio laini wa ndani wenye mpini aje nao (soft broom).
4. Ufagio wa nje aina ya chelewa yenye mpini aje nao.
5. Ufagio wa ndani wenye mpini (Hard broom)
6. Fyekeo
7. Dawa ya chooni ya maji lita 5 aje nayo, kwa mwaka
8. Squizer yenye mpini, moja aje nayo

**<u>F. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE:</u>**

A. **Mambo ambayo mwanafunzi hatakiwi kufanya kabisa akiwa shuleni.**

1. Kuvuta sigara.
2. Kufuga kucha ndefu na nywele ndefu.
3. Kufuga ndevu.
4. Kuvaa mavazi yasio sare rasmi ya shule.
5. Kugombana/Ugomvi.
6. Kuiga mitindo ya kihuni isiyofaa (eg. Kuvaa Kata-K).
7. Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa.
8. Kwenda nje ya shule bila kuvaa sare ya shule.
9. Kwenda nje ya shule bila ruhusa.
10. Kuvaa kofia/Bangili na mapambo mengine yasio sehemu ya sare ya shule.
11. Kuwa na simu, kamera na radio shuleni.
12. Kutembelewa na wageni zaidi ya mara moja kwa mwezi (siku ya jumamosi na jumapili ya kila mwisho wa mwezi).
13. Kula chakula nje ya bwalo bila ruhusa.
14. Kukiuka RATIBA au utaratibu wa shule.
15. Kupeleka wageni bwenini.
16. Kwenda mjini/sentani bila ruhusa maalumu.

17. Kwenda kwenye nyumba za Walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa/sababu ya muhimu.
18. Kula darasani/bwenini.
19. Kunywa pombe ya aina yoyote.
20. Kunyoa kipara.

B. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULEMARA MOJA NI:**

1. Wizi.
2. Uasherati/Ubakaji na Ushoga.
3. Uvutaji bangi.
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya Kulevya/Mihadarati.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau Bendera na Wimbo wa Taifa.
9. Kuoa.
10. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kusaidia kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo zenye kuvuruga amani, usalama wa watu na mali ya umma.
13. Kutoingia katika vipindi/darasani au kukataa kufanya mitihani na mazoezi.
14. Kukataa adhabu kwa makusudi.
15. Mwanafunzi kuwa na Simu ya Mkononi, Redio, Kamera au Tv.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote wa kiume kutembelea mabweni ya wasichana.

**N.B:** Mzazi/Mlezi soma kwa makini sana sheria hizo hapo juu na ukae na kijana wako ukimsisitiza kuzifuata awapo shuleni hasa suala la umiliki wa simu na mgomo.

**Nakutakia kila la kheri Karibu Bukama Sekondari.**

……………………………………..

OKORE R.B

**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI BUKAMA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA**
**SHULE YA SEKONDARI BUKAMA**
**HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Ukoo …………………..Jina la kwanza ………….…. Jina la Kati ……………….…..
2. Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………...…………………...………………...
3. Kama ni Mlezi: Uhusiano …………………………….….. Namba ya simu…………
4. Anwani ya Kudumu ya Mzazi/Mlezi ………………………………..……..……………..…
5. Mahali mwanafunzi alipozaliwa: Mtaa Wa/Kijiji cha …………….…... Kata ya ………..…...
   Wilaya ya ……………………………………………. Mkoa wa ……………………………
6. Dini ………………………………..…….. Dhehebu ……………………..………………...
7. Unaingia Kidato cha …………………..……. Tarehe/Mwaka ……………….……………
8. Kutoka shule ya Sekondari …………………… Wilaya ……………… Mkoa ………………
9. Mzazi wako anafanya kazi ya ajira/Mkulima/Biashara ………………….Mahali ……………
   ………………………………………………………………………………….……….
10. Usafiri kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni: (Toa Maelezo).
    (i) ………………………………………………………………………………….
    (ii) …………………………………………………………………………………
    (iii) ………………………………………………………………………….……….
11. Ndugu Wengine ambao wanaweza kupelekewa habari juu yako/Maswala ya shule ni:-
    (i) ………………… ……………..uhusiano ……………. namba za simu …………………………
    (ii) ………………… ……………..uhusiano ……………. namba za simu …………………………
    (iii) ………………… ……………..uhusiano ……………. namba za simu …………………………
12. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na daktari? Ndiyo/Hapana.
    Ni ugonjwa upi ni wa kudumu kwako? ……………………………………..……………
13. Sifa maalumu kama unazo/yo……………………………………..…….……………..
14. Unalipiwa/Utalipiwa Karo na: (Taja jina anwani yake na namba za simu)
    ……………………………………………………………..…………………………
15. Taarifa za Wazazi wako: Wapo ………………………………….…………………………
    Wamefariki ……………………………………...…. (Weka alama ya vyema panapohusika).

Nakiri kuwa maelezo yaliopo hapo juu ni sahihi.

| | |
|---|---|
| **…………………………………** | **……………………...…….** |
| **SAINI YA MWANAFUNZI** | **SAINI YA MZAZI/MLEZI** |

## HATI YA KUKUBALI:

Mimi (Jina la mwanafunzi) ……………………………………… nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kufuata sheria zote za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

**Saini ya Mwanafunzi …………………………. Tarehe …………………………**

## TAMKO LA MZAZI/MLEZI:

Mimi Mzazi/Mlezi (Jina) ……………………………….. ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi

……………………………..………… nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Bukama ambako Kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza Mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na Uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe Raia bora na mwema wa

Taifa letu.

**Saini ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………Tarehe ………………………..**

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL ADMINISTRATIONS**

**BUKAMASECONDARY SCHOOL**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

***(To be filled by an Authorized Government Medical Officer)***

Full name of Student ……………………………………………………….
Age ……………………..
Height (in cms) ………………………..…… Weight (in kgs)……………………………….

1. Blood count …………………….. (Red and White) ……………….……..
2. Stool Examination ……………………………………………………..…..
3. Urine analysis ……………………………………………………..….
4. Syphilis and other V.D ………………………………………….….........
5. T.B. and Leprosy Test ……………………………………………….….
6. Eye Test ……………………………………………………..……….
7. Ear Test ……………………………………………………………….
8. Chest Test ……………………………………………………….….
9. Abdominal Test ……………………………………………………....
10. Blood Group (very crucial) ……………………………………..………
11. Spleen…………………………………………………………………
12. H.I.V. Test, Positive ………………….…… Negative ……………..……....
    (Tick where necessary)

Additional information e.g. Physical defects or impairment, infections, chronic or family Diseases (e.g. Sickle cell) ………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

I (full name) ……………………………………………… Certify that the above student is fit/is not fit pursue Secondary Education.

Designation ……………………………….
Station ……………………………Signature………………………………….
Date……………………………………... Rubber Stamp ………………………